

Kwa Nini Mungu Anawaacha Watu Wateseke?

(Sehemu ya 1)

Inategemea sura ya 11 ya kitabu *Biblia Inafundisha Nini Hasa?* kinachopatikana kwenye jw.org/sw.

LENGO: Chunguza mambo unayoamini na sababu za kuamini mambo hayo, chunguza kile ambacho Biblia inafundisha, na uone jinsi unavyoweza kuwaeleza wengine mambo unayoamini.



JE, MUNGU NDIYE WA KULAUMIWA KWA SABABU YA KUTESEKA KWETU?

1 CHUNGUZA MAMBO UNAYOAMINI

Kwa nini huenda watu wengine wakasema ndiyo?

Kwa nini huenda watu wengine wakasema hapana?

Wewe unaamini nini?

Kwa nini unaamini hivyo?

2

CHUNGUZA KILE AMBACHO BIBLIA INAFUNDISHA

Yehova hataki tuteseke.

(Ona sura ya 11 ya kitabu *Biblia Inafundisha*, fungu la 1-5.)

Soma 1 Petro 5:7.

Mstari huo unaonyeshaje kwamba Yehova hataki kuona tukiteseka?

Soma Ayubu 34:10.

Je, Mungu anasababisha kuteseka?



Mtengenezaji wa gari hapaswi kulaumiwa dereva anapovunja sheria za barabarani. Vivyo hivyo, Muumba wetu hapaswi kulaumiwa kwa sababu ya matatizo yaliyosababishwa na wanadamu.

Shetani na matokeo ya uasi wake ndiyo yanayosababisha kuteseka.

(Ona sura ya 11 ya kitabu *Biblia Inafundisha*, fungu la 6-9.)

Soma 1 Yohana 5:19; Ufunuo 12:9.

Mistari hiyo inaonyeshaje kwamba Shetani ndiye anayetaka tuteseke?

Soma Mhubiri 4:1; 8:9; 9:11.

Mbali na uvutano wa Shetani, wakati mwingine ni nini hutufanya tuteseke?

Kwa nini unathamini kujua kwamba Mungu hataki tuteseke na kwamba atatusaidia tunapoteseka?

3

ELEZA MAMBO UNAYOAMINI

MTU AKISEMA . . .

Mungu ni mkatili. Anataka watu wateseke.

UNAWEZA KUMJIBU HIVI . . .

Huenda watu wengi wakakubaliana nawe. Lakini mimi ninaamini tofauti kwa sababu . . .

Unaweza kumwonyesha mtu huyo andiko gani?

Ukizingatia maoni yake, unaweza kuelezaje andiko hilo kwa njia yenye kusadikisha?

MTU AKISEMA . . .

Mungu anauongoza ulimwengu, hivyo mambo mabaya yote yanayotokea ni lazima yawe mapenzi yake.

UNAWEZA KUMJIBU HIVI . . .

Dini nyingi zinafundisha hivyo. Lakini mimi naamini kwamba Shetani ndiye mtawala wa ulimwengu huu kwa sababu . . .

Unaweza kumwonyesha mtu huyo andiko gani?

Ukizingatia maoni yake, unaweza kuelezaje andiko hilo kwa njia yenye kusadikisha?
